

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)

Telegram: "MSW"

Simu: + 255 28 2750271

Nukushi: + 255 28 2750376

Barua pepe: *ded@maswadc.go.tz*



S.L.P. 170,

MASWA,
SIMIYU.

Kumb. Na MDC/ADM/5/40/16

17 Mei 2017

TANGAZO KWA UMMA.

KWA:

WANANCHI WOTE,
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA,
S.L.P. 170,
MASWA.

MAONI, MAREKEBISHO NA PINGAMIZI DHIDI YA RASIMU YA SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA, 2017.

*Chini ya Kifungu cha 155 (1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura
ya 287 rekebu la 2010*

Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, inapenda kuwatangazia wakazi na wananchi wote wanaoishi katika Wilaya ya Maswa:

- a. KWAMBA, kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi na usimamizi wa shughuli zake kwa mujibu wa Mamlaka yake kisheria, Halmashauri ya Wilaya ya Maswa inakusudia kutunga Sheria Ndogo mbili (2) ambazo ni:

- 1. Sheria Ndogo (Ada Na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Maswa za Mwaka 2017**

2. Sheria Ndogo (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Maswa za Mwaka 2017,

- b. KWAMBA, Kwa mujibu wa Ibara ya 18 (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 (rekebu la 2005) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 155 (1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 (rekebu la 2010), Halmashauri ya Wilaya ya Maswa inakaribisha **Maoni, Marekebisho au Pingamizi** dhidi ya rasimu hizo kutoka kwa mtu au Taasisi yoyote iliyo katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Maswa.
- c. KWAMBA, Nakala za rasimu za Sheria Ndogo hizo zimewasilishwa kwenye Ofisi zote za Maafisa Watendaji wa Kata kwa ajili ya kujadiliwa na Kamati ya maendeleo ya Kata (WDCs). Wananchi wote wanaweza kuzisoma rasimu hizo katika Ofisi za Kata.
- d. KWAMBA, pingamizi au maoni yoyote yatatakiwa kuwasilishwa kwa **maandishi** ndani ya muda wa siku **Kumi na nne (14)** tangu tarehe ya tangazo hili kwa **Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, S.L.P. 170** au katika **Ofisi za Watendaji wa Kata** kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa saa 1: 30 asubuhi hadi saa 9: 30 mchana.
- e. KWAMBA, baada ya siku Kumi na nne (14) za muda wa tangazo hili kupita Halmashauri ya Wilaya ya Maswa **haitapokea** pingamizi au maoni / marekebisho kutoka kwa mtu yeyote na badala yake itaendelea na mchakato wa kupitisha rasimu za Sheria Ndogo hizo.

Imetolewa na

Dr. Frederick D. Sagamiko

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA

Nakala:

1. Mwenyekiti, - kwa taarifa
Halmashauri ya Wilaya ya Maswa,
S.L.P 170,
Maswa.

 2. Mkuu wa Wilaya, - kwa taarifa
Wilaya ya Maswa,
S.L.P 05,
Maswa.

 3. Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Maswa -
<https://www.maswadc.go.tz>

 4. Mbao za Matangazo:
 - Ofisi zote za Watendaji wa Kata,
 - Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Maswa,
 - Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), Maswa,
 - Mahakama ya Mwanzo Nyalikungu, Maswa,
 - Mahakama ya Wilaya ya Maswa,
 - Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Maswa,
 - Soko Kuu Maswa Mjini,
 - Uwanja wa mpira Wa Miguu Nguzo nane,
 - Ofisi zote za Maafisa Tarafa.
 - Soko kuu la Wilaya ya Maswa
-